

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

Simu: +255262963470
Barua Pepe: ps@mit.go.tz
Barua Pepe: gcu@mit.go.tz
Tovuti: www.mit.go.tz
Nukushi: +255262963117



Mji wa Serikali,
Mtumba,
Mtaa wa Viwanda,
S.L.P 2996,
40478, Dodoma.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**FURSA ZA KUWEKEZA KATIKA VIWANDA VILIVYOBINAFISISHWA
NA KUREJESHWA SERIKALINI**

23 Agosti, 2021, DODOMA.

Kama sehemu ya utekelezaji wa sera ya kuipa sekta binafsi fursa ya kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya uchumi wa nchi iliyotekelzeza kuanzia miaka ya 1990, pamoja na mambo mengine, Serikali ilibinafisisha viwanda 156. Moja ya masharti ya kubinafisisha viwanda hivyo katika mikataba ilioingiwa kati ya Serikali na wawekezaji ilikuwa ni kwa wawekezaji kuhakikisha kuwa wanaviendeaza viwanda hivyo kwa tija. Hata hivyo, tathimini iliyofanyika mwaka 2017 ilibainisha kuwa ni viwanda **88** pekee vilivyokuwa vinafanya kazi kwa kuzingatia matakwa ya mikataba husika. Tathimini hii ilionesa pia kuwa viwanda **68** vilikuwa havifanyi kazi kwa mujibu wa mikataba iliyokuwepo. Aidha, kati ya 68 ambavyo vilikuwa havifanyi kazi viwanda **20** vilishapoteza sifa ya kuwa viwanda.

Hivyo, Serikali ipo katika hatua za kurudisha viwanda 48 ambavyo vilibinafisishwa lakini havifanyi kazi kwa mujibu wa mikataba husika kwa hatua zingine za uwekezaji. Hadi sasa Serikali imesharudisha **viwanda 20** ambavyo havina mgogoro wa kisheria na sasa viro tayari kwa uwekezaji mpya. Kupitia taarifa hii, ninatangaza fursa za kuwekeza katika viwanda hivi 20 kwa utaratibu ufuataao:

- i) Viwanda kumi (10) vinatafutiwa wawekezaji wapya kutoka sekta binafsi kwa ajili ya kuvienda;
- ii) Viwanda nane (8) vimekabidhiwa kwa Mamlaka ya Maeneo ya Uzalishaji wa Mauzo ya Nje (EPZA) kwa ajili ya Uwekezaji kwenye Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZ) ambapo EPZA itaandaa utaratibu wa kupata wawekezaji katika maeneo hayo; na
- iii) Viwanda viwili (2) vitakabidhiwa kwa mashirika ya umma ili waviendeze kwa kuingia ubia na wawekezaji wa sekta binafsi. Viwanda hivi ni Mang'ula

Mechanical Machine Tools kilichopo Morogoro (kinakabidhiwa NDC) na Mbeya Ceramics Co. Ltd. (kinakabidhiwa SIDO).

Ninawakaribisha wawekezaji wenye nia na uwezo wa kuwekeza katika maeneo ya viwanda vilivyoainishwa (Tazama majedwali ya hapa chini) kuwasilisha maombi yao kwa Ofisi ya Katibu Mkuu, Wizara ya Viwanda na Biashara. Zoezi hili litafanyika kwa njia ya wazi na ushindani. Taarifa zaidi kuhusu taratibu za kuwasilisha maombi haya zitatolewa kuititia vyombo vya habari.



Prof. Kitila A. Mkumbo (MB)
Waziri wa Viwanda na Biashara

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

**ORODHA YA VIWANDA VILIVYOBINAFISHWA NA KURUDISHWA SERIKALINI
AMBAVYO WANATAFUTIWA WAWEKEZAJI WAPYA**

A: ORODHAYA VIWANDA VINAVYOTAFUTIWA WAWEKEZAJI KWA NJIA YA ZABUNI YA WAZI

| JINA LA KIWANDA | MAHALI KILIGO |
|---|---------------|
| 1. KILIMANJARO PADDY HAULLING COMPANY | KILIMANJARO |
| 2. POLYSACKS COMPANY LTD | DAR ES SALAAM |
| 3. NMC ISAKA RICE MILL COMPANY LIMITED | SHINYANGA |
| 4. MULTIPURPOSE OIL SEED PROCESSING CO. LTD (MOPROCO) | MOROGORO |
| 5. CDA INTERGRATED CONCRETE INDUSTRY | DODOMA |
| 6. MANAWA GENERRIES LTD | MWANZA |
| 7. NMC TABORA RICE MILL | TABORA |
| 8. MUSOMA TEXTILES MILL | MUSOMA |
| 9. NMC MZIZIMA MAIZE MILL | DAR ES SALAAM |
| 10. PESTCIDES MANUFACTURERES LIMITED - MOSHI | KILIMANJARO |

B: ORODHA YA VIWANDA AMBAVYO WAWEKEZAJI WATAPATA FURSA KUPITIA UTARATIBU WA EPZA

| JINA LA KIWANDA | MAHALI KILIGO |
|-------------------------------|---------------|
| 1. MWANZA TANNERIES | MWANZA |
| 2. TPL SHINYANGA MEAT PLANT | SHINYANGA |
| 3. MAFUTA ILULU | LINDI |
| 4. NACHINGWEA CASHEWNUT | LINDI |
| 5. MKATA SAWMILL LIMITED | TANGA |
| 6. TPL MBEYA | MBEYA |
| 7. SIKH SAWMILL LIMITED | TANGA |
| 8. NATIONAL STEEL CORPORATION | DAR ES SALAAM |

C: VIWANDA VITAKAVYOENDELEZWA NA TAASISI ZA SERIKALI KWA KUSHIRIKIANA NA WAWEKEZAJI BINAFSI

| JINA LA KIWANDA | MAHALI KILIGO |
|--|---------------|
| 1. MBEYA CERAMIC LTD | MBEYA |
| 2. MANG'ULA MECHANICAL & MACHINE TOOLS | MOROGORO |

